

Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | July-2026

EAJK

Mikakati ya Upole kwenye Hafla za Mazishi: Mifano Kutoka katika Baadhi ya Jamiilugha za Waluhya

Authors

Kennedy Opindi Ongadi [(1)]; **Magdalene Wafula** [(2)]; **Samwel Obuchi** [(3)]

Main author's email: Kennedyopindiongadi@gmail.com

(1.2.3) Moi University, Kenya.

Cite this article in APA

Ongadi, K. O., Wafula, M., & Obuchi, S. (2026). Mikakati ya upole kwenye hafla za mazishi: Mifano kutoka katika baadhi ya jamiilugha za Waluhya. *Eastern Africa journal of Kiswahili,* 5(1), 79-91. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.1043

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

Article history
Received: 2026-05-21
Accepted: 2026-06-15
Published: 2026-07-06

Scan this QR to read the paper online

Copyright: ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

Ikisiri

Utafiti huu ulichanganua mikakati ya upole katika hafla teule za mazishi miongoni mwa jamiilugha za Waluhya ili kuonyesha inavyochangia katika kukabiliana na matendo ya usemi yaliyotishia nyuso za waombolezaji. Umilisi wa kipragamatiki wa wazungumzaji au upungufu wake unaweza kuathiri mahusiano ya wazungumzaji katika hafla za mazishi. Nadharia ya Upole ya Leech iliyoboreshwa na Alabdali iliongoza utafiti huu. Jumla ya wasailiwa 40 (20 wanawake, 20 wanaume) walishiriki mijadala ya makundi. Aidha, jumla ya mahatibu 48 (12 kutoka katika kila jamiilugha) walifanyiwa uchunzaji walipokuwa wakihutubu katika hafla za mazishi za jamiilugha teule. Data ya utafiti wetu ilikusanywa kupitia uchunzaji shirikishi na mijadala ya makundi. Utafiti wetu ulikuwa wa kithamano uliochanganua data kimaelezo kwa mujibu wa malengo na nadharia za utafiti. Data iliyokusanywa kwa mfumo wa hotuba za wazungumzaji na rekodi za maandishi ya uchunzaji ilisimbwa. Data yenye iliwekwa kwa makundi bainifu kisha ikaratibiwa kimaudhui. Uchanganuzi wa kina wa data ulifanywa kwa mujibu wa malengo na nadharia za utafiti huu. Matokeo ya utafiti yalibainisha mikakati mbalimbali ya upole ambayo mahatibu waliitumia kutolea rambirambi. Mikakati hiyo ilikuwa: upole kama kanuni ya kumsifu msikilizaji; upole kama kanuni ya kujitweza; upole kama kaida ya maafikiano; kanuni ya kutojisifu na upole kama kaida ya huruma. Jamiilugha ya Wabukusu na Ilihitimishwa kuwa iwapo jamiilugha za Waluhya zitazingatia upole, sherehe za mazishi zitaendeshwa kwa amani. Kadhalika, tulihitimisha kuwa wanajamiilugha husika wanafaa kuwa na umilisi wa kipragmatiki wa jamiilugha nyingine wanazotagusana nazo ili waheshimu kanuni za upole. Tafiti za baadaye zinafaa kuchunguza namna mahatibu katika jamiilugha nyingine za Waluhya zinadhihirisha upole.

Maneno muhimu: Mikakati ya upole, hafla za mazishi, jamiilugha za Waluhya, umilisi wa kipragmatiki, Nadharia ya Upole.

UTANGULIZI

Utafiti huu ulichanganua mikakati ya upole iliyojitokeza kwenye hotuba katika hafla teule za mazishi miongoni mwa jamiilugha za Waluhya. Mikakati hiyo ya lugha ni kigezo cha kubainisha umilisi wa kimkakati wa mahatibu katika lugha husika hasa katika kueleza maana za kijamii ipasavyo. Katika hafla za mazishi, wanajamii hutoa rambirambi zao kwa marehemu na wasipozingatia kaida za lugha wanaweza kuwaudhi waombolezaji. Mikakati ya upole tuliyoirejelea ni: upole kama kaida ya mkakati; upole kama kanuni ya kumsifu msikilizaji; upole kama kanuni ya kujitweza; upole kama kaida ya maafikiano; kanuni ya kutojisifu na upole kama kaida ya huruma.

MAPITIO YA MAANDISHI

Dhana ya Kifo

Kifo ni hali ya mtu kufikia hatima ya maisha yake na moyo wake huacha kudunda na hubadilika kutoka umbo la kimwili hadi la kipepo (Ushe (2017). Kifo chochote kinapotokea huwasababishia ndugu, jamaa na marafiki huzuni mkubwa (Shiino, 1997). Paula na Yakobo (2019) walibainisha kuwa kuna vifo vizuri na vifo vibaya katika jamii za kiafrika ambapo vifo vibaya vilihusishwa na mambo kama vile kujitia kitanzi, ajali, mtu akiaga akiwa mseja, mtu akiaga kabla ya kumpata mtoto, kuuawa kinyume cha sheria na kufa kutokana na kushiriki matendo yasiyokuwa ya kimaadili kama vile kuiba. Kwa upande mwingine, Paula na Yakobo walihusisa vifo vizuri na ukongwe, kufia usingizini, kuugua ghafla au kufa kifo kisichokuwa na uchungu. Aina ya kifo cha mtu hudhibiti namna mahatibu watatumia lugha kumwomboleza mfu.

Hafla za Mazishi

Kulingana na Vedavathi (2022), sherehe za mazishi huwa kumbukumbu ya maisha ya aliyeaga dunia na huwafanya wanajamii kumtukuza marehemu kwa heshima kuu. Hii ni kwa sababu, marehemu huwa amekamilisha mambo yake duniani na hataonekana tena. Baadhi ya tafiti (Tazama Cook na Walter, 2005; Manan na Ararifin, 2019). Kwa mfano, Cook na Walter walieleza kuwa sherehe za mazishi za sasa kule Uingereza zina mseto wa mila na tamaduni asilia, kama vile kuiombea roho ya marehemu ipokelewe na Mungu. Hali ni sawa barani Afrika ambapo kuna mseto wa utamaduni wa jamiilugha na ibada katika sherehe za mazishi.

Kuligana na Shiino (1997), hafla za mazishi huandaliwa ili kuwapa fursa ndugu, jamaa na marafiki kutoa rambirambi zao kwa marehemu na kuwa katika hafla za mazishi, hotuba ambazo hutolewa na wazazi, ndugu na dada, wanawe na marafiki sharti zionyeshe upole, faraja kwa waliofiwa, uzalendo, heshima za mwisho kwa mfu, kutambua mchango wa mfu kwa jamii na kutoa maombi ili roho ya mfu ipokelewe vyema peponi. Isiko na Serugo (2021) wanaeleza kuwa baadhi ya watu mashuhuri katika jamii walipoaga, jamii yake ingemchinjia fahali au hata nyati kumtukuza.

Uchunguzi wa Mmandike na Egenti na (2016) ulionyesha kuwa lazima marehemu azikwe kwa kuzingatia desturi za mazishi za jamii husika. Isiko na Maate (2019) wanaeleza kuwa baadhi ya mila na desturi za mazishi zililenga kuwatuliza waliofiwa ili waweze kukabiliana na ugumu wa kumpoteza mpendwa wao.

Sherehe za mazishi nchini Kenya zinatofautiana kutoka kwa jamiilugha moja hadi nyingine. Kulingana na Ogola (2015), maandalizi ya mazishi mazuri na ya kitaadhima katika jamiilugha ya *Wajaluo* ilikuwa njia mojawapo ya kuonyesha kuwa mwendazake aliheshimiwa na kupendwa na wanajamii. Jamiilugha husika iliandaa sherehe ya 'taraburu' kumwomboleza mfu ambapo waombolezaji walipiga mimea na chochote walichokumbana nacho kuonyesha uchungu wao. Ogola aliongeza kuwa waombolezaji walitoa sifa chanya za marehemu katika hotuba zao kama vile: "Alikuwa mtu mwema, karimu, alikuwa na mlahaka mwema na majirani na mpenda maendeleo ili kuashiria upole. Hata hivyo, si kila wakati ambapo mahatibu katika sherehe za mazishi huzingatia lugha ya upole. Isitoshe, si kila Mjaluo ambaye huandaa sherehe za kitaadhima za mazishi kwa sababu ya umaskini.

Korir (2021) alieleza kuwa jamiilugha ya sasa ya *Nandi* imeanza kuwaandalia marehemu sherehe za kitaadhima tofauti na hapo kale ambapo mazishi ya marehemu yangefanywa na familia ya mfu pekee yake. Korir aliongeza kuwa mahatibu kwenye sherehe za mazishi huhitajika kutumia lugha inayoonyesha masikitiko, inayowaletea wanaoomboleza faraja na inayomheshimu aliyeaga. Hii inamaanisha kuwa mahatibu kwenye sherehe za mazishi wanafaa wawe na umilisi wa kimawasiliano na wa kimkakati ili kukabiliana na vikwazo vya lugha vinavyotokana na

miiko ya lugha viliyowekewa maneno na kauli katika sherehe za mazishi. Aidha, umilisi huo wa lugha ya mazishi utawawezesha kujizuia kutekeleza vitendo ambavyo vinatisha nyuso za waombolezaji.

Lagat (2022) alibainisha kuwa hafla za mazishi katika jamiilugha za *Waluhya* zilikuwa changamano zaidi kutokana na tofauti za kimila baina ya makundilugha mbalimbali ya *Waluhya* pamoja na imani za *Waluhya* kuwa kifo husababishwa na uchawi, laana na maadui. Kadhalika, Lagat aliongeza kuwa *Waluhya* waliamini kuwa watu hawafi bali husafiri kutoka ulimwengu wa kawaida na kuingia katika ulimwengu mwingine wa kipepo ambapo wana uwezo wa kuyatazama yanayoendelea na kuwaathiri wanaowakasirisha. Imani hizo zinaweza kusababisha migogoro wakati wa mazishi na kudhibiti namna lugha inavyotumiwa na mahatibu mbalimbali kwenye sherehe za mazishi pamoja na waombolezaji. Isitoshe, imani hizo zinaweza kuwashinikiza waobolezaji katika sherehe za mazishi teule za *Waluhya* kuzingatia upole wanapozungumza katika muktadha wa mazishi wakihofia kusumbuliwa na pepo wa marehemu.

Kibigo na wenzake (2019) wanaeleza kuwa wanajamiilugha ya Waisukha iliwaandalia mashujaa wa jamii walioaga hafla ya 'shilemba' iliyohusisha kupiganishwa kwa mafahali kwenye kaburi la marehemu. Sherehe hiyo ilikuwa adimu sana na iliandaliwa watu maarufu peke yao. Hafla hiyo pia ilihusisha unywaji wa pombe aina ya busaa pamoja na ulaji wa makochokocho ya vyakula. Ingawa ni vizuri kuwaandalia mashujaa halfla kubwa, utamaduni huu haukuwatambua mashujaa wa kike katika jamii.

Mwisho, kuna hali katika jamii ambazo zinawazuia wanajamii kutekeleza hafla za mazishi. Andreia (2021) alibainisha kuwa tangu majanga ya magonjwa yatambuliwe na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) Machi, 11, 2020, vifo vya watu duniani viliongezeka maradufu na kuwazuia wanajamii kutimiza mila zilizohusiana na sherehe za mazishi. Kulingana nao, katika kipindi cha UVIKO-19, hatua madhubuti zilichukuliwa na maafisa wa afya na serikali kuzuia maenezi yake na baadhi ya hatua hizo ziliathiri tamaduni zilizohusiana na mazishi.

Kimhutasari, hafla za mazishi huwa jukwaa la kijamii ambapo lugha ya upole hutumika. Ni katika hafla za mazishi ambapo wanajamii huomboleza kwa mujibu wa mila na desturi zao. Vile vile, katika hafla ya mazishi, kuna uwezekano wa baadhi ya wanajamiilugha kuvunja miiko ya lugha na hivyo kusababisha hali ya kutoelewana.

Lugha ya Upole

Dhana ya upole imeelezwa na watafiti mbalimbali. Kulingana na Lakoff (1975), upole ni dhana iliyovumbuliwa katika jamii ili kuzuia migogoro katika mawasiliano ya watu. Lakoff anaonekana kuwianisha upole na maadili ya lugha au kanuni ambayo inafaa kufwatwa na watu. Leech (1983) anajeleza kuwa upole ni mkakati wa kuepuka migogoro ambao unaweza kupimwa kutokana na juhudi ambazo zinatumiwa kuepuka hali ya mgogoro. Leech anaingiza suala la mkakati ambapo upole unatazamwa kuwa suala la kipragmatiki ambalo binadamu wanafaa kulizingatia. Kasper (1990) naye anaeleza kuwa upole ni sehemu ya juhudi za binadamu za kuyafanya mawasiliano kufanikiwa na kuwa ya maridhiano. Nao Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa upole ni mfumo changamano wa kupunguza matendo ya usemi ambayo huathiri nyuso za wazungumziwa. Ufafanuzi huo unarejelea heshima ya kijamii ambayo kila mwanadamu razini anafaa kuwa nayo na angependa watu wengine kuiheshimu.

Utafiti wetu uliongozwa na Nadharia ya Leech ya Upole (1983) ambayo inaangalia upole kutoka kwa mtazamo wa msemaji na msikilizaji. Kulingana na Leech msemaji hutoa ujumbe kwa kimkakati na hutarajia kuwa ujumbe alioulekeza kwa msikilizaji utaeleweka. Leech anaongeza kuwa msikilizaji anafaa kuwa na umilisi wa kimkakati ili aweze kufasili ujumbe alioupokea kutoka kwa msemaji sawa sawa. Katika hafla za mazishi za jamiilugha za Waluhya, kila jamiilugha huwa na mitindo ya kueleza mambo pamoja na miiko iliyowekewa baadhi ya maneno na kauli. Maneno na kauli hizo huelezwa kwa njia mbadala iliyokubalika kijamii. Hii inamaanisha kuwa yeyote ambaye hana umilisi wa mikakati husika anaweza kutengwa katika mawasiliano. Utafiti wetu ulibainisha namna mahatibu wa jamiilugha teule za Waluhya walidhihirisha upole katika hafla za mazishi.

Wataalamu wa Isimujamii na Uamali wametambua uhusiano wa karibu mno kati ya umilisi wa kimawasiliano na umilisi wa kimkakati katika

kupambanua mawasiliano ya kijamii. Halliday (1978) alisisitiza kuwa sarufi sharti ieleze kwa maneno mifanyiko na maarifa ya jamii husika. Ule wezo wa kuelewa kilichokusudiwa na mzungumzaji huitwa umilisi wa kimkakati na ni sehemu ya umilisi wa kimawasiliano ambayo humwezesha mtu kushiriki katika mahusiano ya kijamii (Al- Tayib, 2006). Katika muktadha wa sherehe za mazishi, mahatibu wanafaa watumie lugha ya upole ambayo imetanda maneno ya kuleta faraja kwa waombolezaji na kumkubuka marehemu kwa njia ya mapatano. Inafaa pia wazungumzaji wajiepushe na matendo ya usemi ambayo yanaweza kutishia nyuso zao kwa kutumia mikakati ya upole.

Tafiti nyingine zimeonyesha kaida za upole katika hafla za mazishi mbalimbali ulimwenguni. Vedavathi (2022) alishadidia umuhimu wa kuzingatia lugha ya upole katika hafla za mazishi alieleza kuwa lugha ya upole huwasaidia waombolezaji kutuliza uchungu wa kumpoteza mmoja wao kando na kutoa fursa kwa watu wengine kuisaidia familia ya mwendazake. Kulingana na Singal et al (2018) alieleza kuwa jamii huzingatia mila na utamaduni katika hafla za mazishi. Kulingana nao, jamii imewekea miiko ya lugha baadhi ya maneno na kauli zinazofaa kutumiwa au kutotumiwa katika hafla za mazishi. Kulingana na Singal et al, hafla za mazishi ziliandaliwa wakati mtu alikufa ili kuwawezesha waombolezaji kufarijika na kupata nguvu ya kuyaendeleza maisha.

Utafiti wa Owiredu (2020) ulionyesha kuwa jamii za Waafrika zilitumia lugha ya upole ya kuokoa 'uso' wa msikilizaji ili kuifariji familia ya marehemu, kueleza sifa za marehemu na mambo mazuri aliyoyatimiza maishani. Mtazamo wake hata hivyo ulikuwa wa kijumla sana na haukutambua kuwa kila jamii ina njia yake ya kuonyesha upole. Isitoshe, Mmandike na Egenti walisisitiza kuwa mahatibu kwenye sherehe za mazishi wanafaa kusifia mambo mazuri aliyoyafanya mwendazake pamoja na jumbe za kumtakia mema alikoenda maana sifa nzuri ndizo humpa mwendazake heshima. Hata hivyo, inawezekana kwa baadhi ya mahatibu kwenye sherehe za mazishi kutekeleza matendo ya usemi ambayo yanatishia nyuso za waombolezaji, hivyo kuzua haja ya kutumia mikakati ya upole kuwarejeshea walengwa nyuso chanya.

Kwa mujibu wa Isiko na Serugo (2021), jamiilugha ya *Wasoga* ilihuzunishwa wakati kifo cha mtu maarufu na mwadilifu katika jamii kilipotokea. Kulingana nao, Wasoga walimwoboleza marehemu kwa maneno ya kuonyesha uchungu kama vile 'amekataa kula chakula', 'Ndio mara ya mwisho ya kumwona.' Waliongeza kuwa hotuba za mahatibu katika sherehe za mazishi zilitumiwa kuwachochea watu walio hai kuiga matendo mazuri ya marehemu. Kwa njia hiyo, jamiilugha husika ilihifadhi uso hasi wa mfu wakati wa kumwomboleza. Isiko na Serugo walipinga hali ya baadhi ya mahatibu kumhukumu marehemu hadharani maana huwa amefikia hatima ya maisha yake na kwa kufanya hivyo kungeiudhi jamaa yake. Licha ya utafiti huo kusifia matendo mema ya mfu, inafaa matendo mabaya ya mwendazake yakashifiwe ili kuiadilisha jamii.

Hatabarat (2021) alieleza kwamba watu wanafaa kulinda 'nyuso' zao dhidi ya mambo ambayo yanayoweza kuutishia uso chanya wa msikilizaji kama vile hisia za chuki, lawama, matusi, vitisho, na tahadhari wanapozungumza. Kulingana na Hatabarat, masuala hayo yanaweza kuyakatiza mawasiliano au hata kuzua vurugu. Katika muktadha wa sherehe za mazishi, hisia za kupindukia zinaweza kuibuka na kuwafanya wanaohusika kutekeleza vitendo ambavyo vinaweza kutishia nyuso za waombolezaji katika sherehe za mazishi.

Ongunyemi (2007) alisisitiza kuwa upokezi wa maadili ya kijamii ni mojawapo wa majukumu ya lazima ya kila mwanajamii mzima. Hii ni kwa sababu, watu wazima huwa na umilisi wa kutosha wa sarufi na mikakati ya lugha zao. Kadhalika, watu wazima wasipotetea maadili ya kijamii, kizazi kizima kinaweza kupotoka. Kuhudhuria sherehe za mazishi mara kwa mara humwezesha mwanajamii kupokea umilisi wa kimawasiliano pamoja na umilisi wa kimkakati wa sajili ya mazishini. Hata hivyo, huenda utamaduni huo wa lugha umefifia au umeathiriwa na tamaduni za jamiilugha nyingine.

Mintaarafu ya maandishi ya wataalamu tuliyoyarejelea, masuala kadhaa yanaibuka: Je, ni maneno na kauli zipi zilizowekewa miiko ya lugha katika sherehe za mazishi miongoni mwa jamiilugha za *Waluhya*? Je, jamiilugha za Waluhya hutumia mikakati ipi ya upole katika sherehe za mazishi? Je, ni mambo yepi ambayo

hutishia 'nyuso' za marehemu katika sherehe za mazishi miongoni mwa jamiilugha husika? Mwisho, jamii za *Waluhya* huzingatia upole hasi au upole chanya katika sherehe za mazishi?

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti wetu ulikuwa wa kithamano. Hususan, tulichanganua data yetu kimaelezo kwa mujibu wa malengo na nadharia ya utafiti. Jumla ya wasailiwa 40 (20 wanawake, 20 wanaume) walishiriki mijadala ya makundi na mahatibu 48 (12 kutoka katika kila jamiilugha) walifanyiwa uchunzaji walipokuwa wakihutubu katika hafla za mazishi za jamiilugha teule. Data ya utafiti wetu ilikusanywa kupitia uchunzaji shirikishi na mijadala ya makundi.

Ili kuchunguza mikakati ya upole na matendo ya usemi yanayotishia nyuso katika jamiilugha teule za Waluhya katika hafla za mazishi, tulichanganua hotuba za mahatibu. Nadharia ya Upole ya Leech (1989) ilitumiwa kama msingi wa uchanganuzi. Nadharia hiyo inahusu dhana ya 'uso' ambao ndio heshima ya mwanajamii ambayo angependa idumishwe. Kulingana na Brown na Levison (1978) uso una sehemu mbili: Uso hasi (Uhuru wa kutenda na wa kutoshurutishwa) na uso chanya (Haja ya mwanajamii ya kuheshimiwa na kutambuliwa na wengine). Kwa hivyo, mikakati ya chanya ya upole huelekezewa mahitaji chanya ya uso kama vile udugu na utambulisho wa mwanakundindani. Kwa upande mwingine, mikakati hasi ya upole huelekezewa mahitaji hasi ya uso kwa kuonyesha urasmi na masafa marefu.

Katika mawasiliano, watu hushirikiana katika kutimiza upole kwa kujitahidi kuhifadhi uso- heshima yao na ya watu wengine. Katika hafla za mazishi, mahatibu huonyesha masikitiko yao kwa kutumia maneno ya kumsifia marehemu, kuonyesha masikitiko na katika uzi ule ule kukumbuka mambo mazuri ambayo marehemu aliyatekeleza maishani.

Ili kuratibu na kuchanganua mikakati ya upole iliyodhihirika kwenye hotuba za mahatibu, tulifwata uanishaji wa Leech wa mikakati ya lugha. Kaida tano za upole zilizoambatana na hafla za mazsihi zilitumiwa: upole kama kanuni ya kumsifu msikilizaji; upole kama kanuni ya kujitweza**;** upole kama kaida ya maafikiano; kanuni ya kutojisifu na upole kama kaida ya huruma. Kila kaida ya upole ilipewa msimbo ili kutusaidia kuratibu data. Baadaye, tulipanga data katika makundi bainifu yenye sifa sawa. Uchanganuzi wa kina wa data ulifanywa kwa mujibu wa malengo na nadharia za utafiti huu.

MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti wetu ulionyesha kuwa mahatibu mbalimbali katika sherehe za mazishi za jamiilugha teule za Waluhya ziliheshimu mikakati ya upole iliyoasisiwa na Leech (1983) walipokuwa wakitoa rambirambi zao kwenye sherehe teule za mazishi za utafiti huu. Mikakati hiyo ya upole ilikuwa: upole kama kaida ya mkakati; upole kama kanuni ya kumsifu msikilizaji; upole kama kanuni ya kujitweza**;** upole kama kaida ya maafikiano; kanuni ya kutojisifu na upole kama kaida ya huruma.

Upole Kama Kaida ya Mkakati

Kaida hii hudhihirika pale ambapo msemaji hutumia kauli ya kupunguza faida kwa nafsi yake ili ajiongezee haiba (Kitamura, 2000). Katika mfano 1, hatibu MH2 alimkweza X kwa kuonyesha ushupavu wake katika biashara licha ya kuwa na kiwango kidogo cha masomo. Alisema:

Mfano 1

LUB: Nende busomi bwewe butiti obwo, X kaba akhola bibiasara. Nechile khusikhha X sikila abele *special*, mupilekho chindayi.

KIS: Na kiwango chake kidogo cha elimu, X alikuwa mwanabiashara. Nimekuja kumzika X kwa kuwa yeye ni spesheli, mpigie makofi.

Hii inamaanisha kuwa X alikuwa maarufu na mkakamavu katika biashara na ndio alitambuliwa na kualikwa kuongoza mchango wa pesa. Mkakati huo wa ulimwongezea X thamani na kuinua haiba yake katika jamii. MH2 anaongeza kusema, "Nichele khusikhha X sikila abele *special*, mukhubilekho chindayi."- Nimekuja kumzika X kwa kuwa yeye ni spesheli, mpigie makofi. MH2 alisifia na kushangilia mafanikio ya X. MH2 aliwaagiza waombolezaji wampigie X makofi kuonyesha kuwa alikuwa ametenda jambo zuri. Kawaida mtu ambaye huwa amefaulu katika jambo fulani maishani ndiye hupigiwa makofi. Alisema:

Katika mfano 2, hatibu MH1 alionyesha heshima kwa wasikilizaji kwa kuwasalimu kwa njia ya kipekee kwa kuyatambua makundi yaliyokuwepo . Alisema:

Mfano 2
LUB: Efamili ya omusale wefwe, X, omukhaye wewe, Y, ekanisa, biongosi, mulembe? Mulembe lundi? Mulembe swaa? Mulembe tee? Muli mwoyo?

KIS: Familia ya rafiki yetu, X, mke wake, Y, kanisa, viongozi, hamjambo? Hamjambo tena? Hamjambo swaa? Hamjambo tee? Mko hai?

Hatibu MH1 alionyesha heshima kubwa kwa kuyatambua makundi yaliyokuwepo kwa kuzingatia itifaki. Utabulisho wa waliokuwepo uliwafanya warejelewa kuhisi vizuri. MH1 alisisitiza salamu hizo ili awachangamshe waliokuwepo na kuivutia nathari yao. Isitoshe, salamu za hatibu MH1 zilionyesha upekee wa salamu katika jamiilugha ya Babukusu. Neno 'mulembe' katika jamiilugha ya Babukusu linamaanisha, 'amani'na kusisitizwa kwa neno hilo na mzungumzaji kumaanisha kuwa wanaohusika katika mazungumzo wanafaa wayaendeshe mazungumzo yao kwa njia ya mapatano.

Upole Kama Kaida ya Kumsifu Msikilizaji
Kaida hii ya upole hudhihirika pale ambapo msemaji huzidisha kauli zinazotoa sifa kwa msikilizaji na kupunguza kauli zisizomsifu msikilizaji. Ili kutimiza lengo hili, msemaji anaweza kutumia tasfida ili kumfanya msikilizaji ajihisi vizuri.

Katika mfano 3, hatibu MH1 alimtambua X kuwa rafiki yake wa dhati na alieleza kuwa waliwahi kufanya naye mchango wa kujenga kanisa la Jeshi la Wokovu. Alisema:

Kauli ya MH1, ilimsawiri X kuwa mtu maarufu katika jamii maana alikuwa mmoja kati ya wageni wa heshima walioalikwa kuchagisha pesa. Alisema:

Mfano 3
LUB: Nechile ano khubela omusecha okonile ano omusale wase sana. 2013-2014 ndecha Matisi mulikanisa la Jeshi la Wokovu khwakhola harambee.

KIS: Nimekuja hapa kwa sababu mwanaume aliyelala hapo alikuwa rafiki yangu wa toka nitoke. 2013-2014 nilikuja hapa Matisi kwa Kanisa la Jeshi la Wokovu tukafanya harambee na X.

Katika mfano 4, kauli ya hatibu MH2 ilimsifia X. Alisema:

Mfano 4
LUB: Nende busomi bwebwe butiti yobo, X aba akhola biasala. Nechele khusikha X sikila abele special, mukhubilekho chindayi. Aba yasoma bulahi khane aruka sibala sino. X yabele *Chief campaigner* wasee yakila ndabira ikura 2022 naba gavana nesili omwana mutiti.

KIS: Na kiwango chake cha chini cha masomo, X alikuwa akifanya biashara. Angekuwa amesoma vizuri angekuwa anaongoza hii nchi. X alikuwa kiongozi mkuu wa kampeni yangu na aliniwezesha kushinda kura za mwaka wa 2022 nikawa gavana nikiwa na umri mdogo.

MH2 alimsifu X kwa namna mbili. Kwanza, kutokana na umaarufu wake katika biashara. MH2 pia alimsifia X kwa kumsaidia kufanya kampeni za kura za mwaka wa 2022 ambapo aliibuka kuwa mshindi. Kwa kutoa kauli hizo, MH2 alitumia kaida ya kusifu kutoa rambirambi yake katika sherehe ya mazishi ya X. Alisema:

Upole Kama Kaida ya Kujitweza
Kanuni hii hudhirihirika pale ambapo msemaji hutumia kauli ambazo zinamtweza huku akipunguza zile ambazo zinamsifu ili anufaike. Msemaji huteua kauli ambazo zinamchochea msikilizaji kumhurumia au kumsaidia.

Katika mfano 5, hatibu MH5 alitumia mkakati wa kujitweza kuonyesha usuhuba aliokuwa nao na X. Alisema:

Mfano 5
LUB: Ese bandu bakali bapara ese wandai wa X. Busale bwakila khufwanana. X kenda bulahi. Uno afwile *accident* butsa. Khulikwima kwe moni khukuree muntsu, kwa mapesa na upendo.

KIS: Mimi watu wengi wanafikiri nina ukoo na X. Ni urafiki ambao umetufanya kufanana. X tembea vizuri.

Huyu ameaga kwa ajali tu. Tutamtafuta mwanamume mwajibikaji tumlete kwa nyumba, mwenye pesa na upendo.

MH5 angependa mjane asitamauke bali achukue hatua ya kuyaanza maisha upya. MH5 alimwandaa mjane kumtafuta mume mwenye uwezo fedha mkubwa ambaye angemtunza pamoja na wanawe. Anajenga mazingira mazuri ya wanaume kuanza kumtafuta mjane wa X maana anasisitiza kuwa kifo cha X kilitokana na ajali. Alisema:

Katika mfano 6 unaofuata, upole kama kanuni ya kujitweza unadhihirika katika kauli ya MH13 alipomshawishi mjane amwoe mke mwingine ambaye angemsaidia kuwalinda wanawe. Alisema:

Mfano 6

LUB: Omwana yuno kanyola omwana wasee omulayi lundi omuolu. Omundu okhenyile Y anyole omundu alinde babana ba X akhilwe lukali! Nono papa ese khusaya olume kabisa. Obukule babana obaile Kibabii balotenge ewase. Mala ewewe oile omukhasi okundi babana bakhule. Nekhuloma khuri khukhulekhele babana sebalakhula nende furaha tawe. Sai khusaba khuli Wele akhuyete onyole omundu omulahi olanga babana lisina lilai. Wele akhuchibe liliekomba lioo lukali. Omwana mawe nafwile akhulilanga ebukukhuwe.

KI|S: Huyu mtoto alimpata kijana yangu mzuri na mpole. Mtu ambaye hataki Y amwoe mtu wa kumsaidia kuwatunza watoto wa X ashindwe kabisa. Sasa baba nakuomba uwe imara. Wachukue wanao upwapeleke Kibabii wasome wakirudi kwangu. Tukisema tukuachie watoto hawatakua na furaha. Saa hii nakuombea Mungu akusaidie umpate mtu mzuri ambaye anaweza kuwapenda wanao. Mungu atajibu vizuri. Mtoto mamake akifa yeye hukulia kwa bibi yake.

MH13 alijitweza alipomkashifu mtu ambaye alimzuia mjane kumwoa mwanamke mwingine. Alikubali kuwa X alikuwa ameshakufa na kuwa hangeweza kurudi tena. Pia alitambua kuwa kazi ya ulezi huwa mzigo kwa wanaume maana wao huwa na shughuli nyingi. Alijitolea kuwalea wanawe Y akimtafuta mtu wa kuoa. Alimkumbusha Y utamaduni wa jamii kuhusu suala la malezi kuwa watoto wakifiwa na mama yao hulelewa na bibi yao. MH13 pia aliyajali mno maslahi ya wajukuu wake. Pia alimshauri Y amtafute mke mzuri ambaye hangewahangaisha wajukuu wake.

Upole Kama Kaida ya Kutojisifu

Msingi wa kaida hii ya upole upo pale ambapo msemaji hupunguza kauli za chuki na kuzidisha kauli za kuwajali watu wengine (Kitamura, 2000). Msemaji huonyesha unyenyekevu kwa kutumia kauli za heshima. Mifano kadhaa ya mkakati huu wa upole ilidhihirika katika kauli za mahatibu kwenye hafla teule za mazishi. Kauli hizi ni: Kauli za Kutaja Mfu, Kauli za Kutaja Kifo, Kauli za heri, Kauli za Kutolea salamu, Kauli za Buriani, Kauli za Kurejelea Unasaba, Kauli za Kutoa Rambirambi na Kauli za Kidini.

Kauli za Heshima za Kumtaja Marehemu

Lagat (2022) alieleza kuwa wakati wa kutoa rambirambi katika hafla za mazishi, watu wa jamiilugha za *Waluhya* humiminia marehemu sifa nzuri kwa upande mmoja kama njia ya kuonyesha heshima yao ya mwisho kwake na hujiepusha kurejelea sifa zake mbaya kwa upande mwingine. Kwa mujibu wa Qanbar (2019), kifo ni mojawapo wa maneno mwiko ambayo hayapaswi kutajwa dhahiri katika mazungumzo kutokana na imani za wanajamii kuwa anayetaja kifo hualika pepo mbaya wa kifo. Kwa sababu hiyo, maneno yanayotaja kifo au marehemu hurejelewa kwa maneno mbadala ya upole ili kukwepa balaa hiyo. Utafiti huu ulibainisha jinsi jamiilugha za *Waluhya* hurejelea marehemu ilivyoonyeshwa na mifano mbalimbali kwenye jedwali 1. Tazama jedwali 3 hapo chini.

Jedwali 1: Kauli za Heshima za Kumrejelea Marehemu

Hatibu	Jamiilugha	Kauli ya Jamiilugha	Tafsiri ya Kiswahili
MH10	LUB	Afwile yoyo ali *cousin* wasee.	Huyo aliyeaga ni binamu yangu.
MH10	LUB	Mukhwasi abele anyolile igolti lakini Wele kachibukule.	Shemeji alikuwa amepata dhahabu lakini Mungu ameichukuwa.
MH13	LUB	Omwana ino kanyola omwana wasee mulahi omuolu.	Huyu mtoto alikuwa amepata kijana yangu mzuri mpole.
MH31	LWI	Yananga *sweety* nintsi mulanga *sweety*.	Alikuwa akiniita sweaty name namwita *sweety*.
MH 31	LWI	Khu ngoristi kulipendwa, mlina wanje, shipenzi shianje shiambilanga *out* mumasitsa.	Kwa hivyo, nimempoteza mpenzi wangu ambaye alikuwa akinipeleka *out*.
MH33	LWI	Akhutsi yali mlina wanje mkali sana.	Aliyeaga alikuwa rafiki yangu mkubwa sana.
MH1	LUB	Nechile hano khubela musecha akonile ano ni musale wase sana.	Nimekuja hapa kwa kuwa mwanamume aliyelala hapa ni rafiki yangu sana.
MH5	LUB	Esese nemeele khukhupa pole khu musale wasee omukosi.	Mimi nimesimama kupiga pole kwa rafiki yangu mzuri sana.
MH14	LUB	Moyo kunchuna nimbona wandase nafuana ario.	Moyo unaniuma nikiona niliyezaliwa naye tumbo moja akifanana hivyo.
MH15	LUT	Intsi nakoritsa musakhulu wanje mweli kwabele.	Mimi nilimpoteza mume wangu mwezi uliopita.

Kauli za Heshima za Kutajia Kifo

Utafiti wetu ulibainisha maneno mbadala yaliyotumiwa na mahatibu katika hafla za mazishi teule kukirejelea kifo. Jambo ambalo lilidhihirika katika utafiti wetu ni kuwa kifo kinaogofia na mahatibu wengi waliotoa rambirambi zao walitumia maneno mbadala kukirejelea. Tazama jedwali 4.

4.

Jedwali 2: Kauli za Heshima za Kutaja Kifo

Hatibu	Jamiilugha	Kauli ya Jamiilugha	Tafsiri ya Kiswahili
MH11	LUB	Yakosisie kila ndalo kila ndalo.	Amekuwa akipoteza kila mwaka.
MH11	LUB	Indalo ino, mai wasingilenge bibindu kachile.	Wakati huu, mama ambaye amekuwa akiosha vyombo ameenda.
MH5	LUB	Nenya khubolela senge Y pole nende bamenya bo musibala sino. X kachile khukorwa khukhole khuriena tawe.	Ningependa kumwaeleza shangazi Y pole pamoja na wakazi wa shemu hizi. X ameenda sijui tutafanyaje.
MH14	LUB	Moyo kunchuna nimbona wandase nafuana ario.	Moyo unaniuma nikimwona niliyezaliwa naye akifanana hivyo.
MH10	LUB	Aba ali lifua liakhupanga hodi, khane khwakhupa ekura X abule khuchia tawe.	Ingekuwa kwamba kifo kingekuwa kinapiga hodi, tungepiga kura X huenda hangeenda.
MH11	LUB	Papa pole kano kamarafu lakini ikhalilikha. Wele amanyile kakholile. Papa kalaha, Mwana wefwe X akende bulahi.	Baba pole, haya ni magumu lakini vumilia. Mungu amejua alichokifanya. Baba pole, mtoto wetu X atembee vizuri.
MH17	LUT	Nibubeleli khukoritsi khotsa weru yakhuyantsa.	Ni huzuni tumempoteza mjomba wetu tuliyempenda.

Kauli za Heshima za Heri

Katika hafla za mazishi za jamiilugha teule, mahatibu mbalimbali walitoa kauli za kuwatakia waliofiwa na marehemu heri. Kulikuwa na kauli za kuliwaza, kujuta, amani, ushauri, tahadhari, lawama, ahadi za kutoa usaidizi na masikitiko kama ilivyoonyeshwa katika jedwali 3 hapo chini.

Jedwali 3: Kauli za Heshima za Heri

Hatibu	Jamiilugha	Kauli ya Jamiilugha	Tafsiri ya Kiswahili
MH1	LUB	Mala nechile khusikha X na nenya khurusia pole yase khu Y ne bana, ekanisa, Batecho na Watebulani.	Nimekuja kumzika X na ningependa kutoa pole kwa Y na watoto, Watecho na Watebulani.
MH2	LUB	Pole mayi, Nyasaye amree X ahehe ahalahi.	Pole mama, Mungu amweke X mahali pake pazuri.
MH4	LUB	Nenya mbukule nafasi ino khupilekho Y pole.	Ningepoenda kuchukua nafasi hii kumpigia Y pole.
MH4	LUB	Kalaha mutinye mu Yesu.	Pole muwe imara kwa Yesu.
MH5	LUB	Esese nemile khukhupa pole khu musale wasee mukosi.	Mimi nimesimama kupiga pole kwa rafiki yangu mwenye heshima.
MH5	LUB	Nenya khubolela senge Y pole nende bamenya bo musibala sino. X kachile khukorwa khukhole khuriena tawe. Tunaomba roho mtakatifu awaongoze.	Ningependa kumwaeleza shangazi Y pole pamoja na wakazi wa sehemu hizi. X ameenda sijui tutafanyaje. Tunaomba roho mtakatifu awaongoze.
MH6	LUB	Mubarikiwe sana. Wemwikulu akasitse lukendo lwa X mwikulu.	Mbarikiwe sana. Mungu abariki safari ya X.
MH10	LUB	Aba ali lifua liakhupanga hodi, khane khwakhupa ekura X abule khuchia tawe.	Ingekuwa kwamba kifo kingekuwa kinapiga hodi, tungepiga kura X huenda hangeenda.

Kauli za Heshima za Kutolea Salamu
Utafiti wetu ulibainisha mitindo ya salamu ambazo hutumiwa katika hafla za mazishi ya jamiilugha za *Waluhya*. Salamu hizo ziliwekwa katika makundi ya salamu za unasaba, dini na waliofika kuomboleza, salamu zilizodhihirisha majina ya unasaba badala ya majina halisi kwa kuwa matumizi ya majina halisi yamewekewa mwiko.

Jedwali 4: Kauli za Heshima za Kutolea Salamu

Hatibu	Kauli ya Jamiilugha	Tafsiri ya Kiswahili
MH3	Bamasika nabakhesiesie mulembe? Mulembe lundi? Mulembe kwa X!	Waombolezaji hamjambo? Hamjambo tena? Slalamu za X?
MH4	Bana befwe mulembe? Mulembe swaa! Mulembe tee?	Ndugu zangu hamjambo? Hamjambo swaa? Hamjambo tee?
MH14	Basenge, bapapa na bamai Muriena?	Akina shangazi, akina baba na akina mama hamjambo?
MH15	Bosi bamwitsi khulila X milembe? Bwana Yesu asifiwe?	Nyote mliokuja kumwomboleza X hamjambo? Bwana Yesu asifiwe?
MH18	Bwali bwa ADC na bosi mwitsi khukhuboa mkoye milembe?	Madhebahu ya kanisa la ADC na wote mliokuja kutufunga Kamba hamjambo?
MH20	Bwali butakatifu, bosi bitsi khukhukhonya malika milembe!	Madhebahu matakatifu, nyote mlikuja kutusaidia matanga, hamjambo?
MH24	Milembe bosi! Milembe cha Mulamwa?	Hamjambo nyote? Salamu za shemeji?
MH25	Milembe bosi? Milembe chi shibelo? Milembe cha basanji?	Hamjambo nyote? Salamu za huzuni? Salamu za kivyera?
MH28	Milembe bosi! Milembe cha malika?	Hamjambo nyote? Salamu za matanga?
MH37	Bosi haleluya! Milembe chia X! Milembe chiu muyantsi wanje X?	Nyote Halelluya? Salamu za X? Salamu za mpenzi wangu X?

Kauli za Heshima za Kutolea Buriani
Katika hafla za mazishi teule, mahatibu wengi walitoa kauli za kumuaga marehemu kwa kuwa hiyo ndio mara ya mwisho ya kuonana naye hapa duniani.

Jedwali 5: Kauli za Heshima za Kutolea Buriani

Hatibu	Jamiilugha	Kauli ya Jamiilugha Husika	Tafsiri ya Kiswahili
MH6	LUT	Wemwikulu akasitse lukendo lwa X mwikulu.	Mwenye mbingu atakase safari ya X ya kuelekea mbinguni.
MH11	LUB	Mwana wefwe X akende bulahi.	Mtoto wetu X atembee vyema.
MH13	LUB	Wele amwikhasie mundebe itakatifu sikila ali omwana omwolu, omwana oli nokumulembe, omwana ochekha kalaha, ali omwana omunamuna, omwana wasima khwing'ona	Mungu amketishe kwa kiti kitakatifu kwa kuwa alikuwa mtoto mpole, mtoto mcheshi, mtoto ambaye haogopi na mtoto ambaye anapenda kujitunza.
MH15	LUT	Mbola pole Nyasaye akasitsi luchendo lwo musakhulu.	Nasema pole na Mungu abariki safari yam zee.
MH20	LUT	Kwamuyantsa lakini Nyasaye anyala vyosi yamuyantsa sana.	Tulimpenda lakini Mungu anayeweza vyote alimpenda sana.
MH23	LUT	Mbola pole khukoritsa X na Nyasaye akasitse luchendo lwelwe.	Nasema pole kumpoteza X na Mungu abariki safari yake.
MH24	LUT	X shiatsili butswa tawe, aleshi bana. Shianyala khurelwa butamanu tawe. Bana mulindi mama wenyu na mumenye mwisala.	X hakuenda bure, aliacha watoto. Hawezi akazikwa vibaya. Watoto mlinde mama yenu na mdumu kwa sala.

Kauli za Kidini za Kutolea Rambirambi
Jamiilugha teule za *Waluhya* zilizotafitiwa zimeathiriwa na dini ya Ukristo. Utafiti wetu uligundua kuwa kanisa ndilo lilioongoza ibada za mazishi. Kwa hivyo, kauli nyingi za mahatibu zilikuwa za heshima.

Kauli za Kumwomba Mungu Amhurumie Marehemu
Katika mfano 7, MH2 alipotoa rambirambi yake kwa mjane alisema, "Pole mayi, Nyasaye amree X ahehe halahi."- Pole mama, Mungu amweke X mahali pake pazuri. Mawazo ya MH2 yaliambatana na mafunzo ya *Biblia* kuwa Mungu humchukua binadamu siku yake ikifika na kuwa siku ya hukumu itakapofika, kila mtu atahukumiwa kulingana na makosa yake (Matayo 13). Kadhalika, binadamu kisilika ni mtenda dhambi na huhitajika kutubu dhambi zake kila mara. Kwa kumjali X, MH2 alimwomba Mungu amweke X mahali pema ambapo hangehangaika. Alisema:

Mfano 7
LUB: Pole mayi, Nyasaye amree X ahehe halai.

KIS: Pole mama, Mungu amweke X mahali pake pazuri.

Kauli za Kumwomba Mungu Ulinzi
Katika mfano 8, MH3 alimhimiza mjane kuwa asihisi upweke maana Mungu ndiye huwalinda wajane na mayatima. Alisema, "Y Omwami wa banamulekhwa nende bafubi alakhunyalila alakhulinda. Olilile mu Kristo."- Y Mungu wa wajane na mayatima atakushindia na atakulinda. Omboleza ndani ya Yesu. Kauli ya MH3 ni ya kumhimiza mjane adumu katika sala maana Mungu huwa na njia ya kuwasaidia wajane na mayatima kumaliza matatizo yanayomkumba. Hata ingawa ushauri wa MH3 ulikuwa mzuri, hajaeleza bayana jinsi Mungu angeweza kumkomboa Y kutokana na pengo lililoachwa baada ya X kuanga. Alisema:

Mfano 8
LUB: Y Omwami wa banamulekhwa nende bafubi alakhunyalila alakhulinda. Olilile mu Kristo.

KIS: Y Mungu wa wajane na mayatima atakushindia na atakulinda. Omboleza ndani ya Yesu.

Kauli za Kuiombea Familia
Katika mfano 9, MH3 anaendelea kumwombea mjane dua anaposema, "Khusabila Nyasaye akhue kamani olinde abana."- Nakuombea Mungu akulinde akupe nguvu za kuwatunza wanao. MH3 anadhihirisha kuwa maisha ya wanadamu yanadhibitiwa na Mungu ambaye ana uwezo, mkubwa. Mungu ana uwezo wa kumlinda mjane na kumpa nguvu. Akiwa katika hali nzuri, MH3 ataweza kuwatunza wanawe. Alisema:

Mfano 9
LUB: Khusabila Nyasaye akhue kamani olinde abana.

KIS: Nakuombea Mungu akulinde akupe nguvu za kuwatunza wanao.

Kauli za Kumwombea Marehemu Dua
Katika mfano 10, MH21 alimwombea X dua katika safari yake. Kauli ya MH21 ni ya kumwombea X baraka katika safari yake. Huenda chanzo cha mawazo hayo ni woga kuhusu hatima ya X alikoenda. Huenda alikuwa mtenda dhambi ambaye angeadhibiwa na Mungu kwa kutupwa motoni.

Kwa kumwombea X dua kwa Mwenyezi Mungu, MH21 alidhamiria kuwa Mungu angemhurumia X na kumruhusu kwenye ufalme wake wa mbinguni. Alisema:

Mfano 10
LWI: Mbola pole, Nyasaye akasitsi luchendo lwa X.

KIS: Nasema pole, Mungu abariki safari ya X.

Kauli za Matumaini ya Kukutana na Marehemu Kuzimuni
Katika mfano, 11, hatibu MH31 alipotoa rambirambi yake alisema angekutana na X kuzimuni siku yake ikifika. Jambo hilo liliashiria kuwa kifo ni tukio la lazima kwa kila mtu ijapokuwahutofautiana kisiku, kisaa na mahali.

Hata hivyo, woga wa MH13 ulimfanya amwombee kwa Mungu atengeneze safari ya X. MH31 alisema:

Mfano 11
LWI: Nyasaye alombe luchendo lwelwe, khulibukana imakombe inyinga lwa niitushe.

KIS: Mungu abariki safari yake, tutakutana kuzimuni siku itakapofika.

Kauli za Kumwomba Mungu Amwadhibu Muuaji wa X
Katika mfano 12, MH14 alisikitishwa na kifo cha X. Aliamini kuwa Mungu alikuwa na uwezo wa kumwadhibu aliyesababisha kifo chake. Kauli ya MH14 inaonyesha jinsi jamiilugha huhusisha kifo na binadamu hasa maadui wa X. Kifo cha X kilitokana na ajali ya moto lakini bado kulikuwa na imani kuwa kifo hicho huenda kilihusishwa na binadamu labda kwa njia ya uchawi. MH14 alisema:

Mfano 12
LUB: Nali binadamu kakilile nafauna ario, Wele amubone

KIS: Ikiwa binadamu ndiye aliyemfanya afanane hivyo, Mungu amwone.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO
Hitimisho: Utafiti huu ulihitimisha kuwa iwapo jamiilugha za Waluhya zitazingatia mikakati ya upole katika hafla za mazishi, basi kutatokea mazungumzo ya mapatano. Kadhalika, ulihitisha kuwa kuna haja ya jamiilugha za Waluhya kuwa na umilisi wa kimkakati wa kipragmatiki wa jamiilugha mbalimbali ili waweze kuwasiliana kwa njia inayokubalika katika hafla za mazishi.

Mapendekezo: Utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe kwenye jamiilugha zingine za Waluhya ili kubainisha mikakati ya lugha wanayoitumia kwenye hafla za mazishi. Utafiti ufanywe kuchunguza iwapo miktadha ya dini na ya kitamaduni inaathiri matumizi ya lugha katika hafla za mazishi katika jamiilugha nyingine za Waluhya.

MAREJELEO

Alabdali, T. S. (2019). Revisiting Brown and Levinson's politeness theory: A Middle-Eastern perspective. *Bulletin of Advanced English Studies, 2*(2), 73–78. https://doi.org/10.31559/baes2019.2.2.3

Al-Tayib Omar, A. M. (2006). The speech act of complaint as realized by advanced Sudanese learners of English. *Journal of Educational and Social Sciences and Humanities, 18*(2), 9–40.

Andrea, B., Solt, S., & Burnett, H. (2022). Context, (im) precision, and social perception: A socio-pragmatic study. *Language in Society, 38*.

Brown, P., & Levinson, S. C. (1978). Universals in language usage: Politeness phenomena. In E. N. Goody (Ed.), *Questions and politeness: Strategies in social interaction* (pp. 56–289). Cambridge University Press.

Brown, P., & Levinson, S. C. (1987). *Politeness: Some universals in language usage*. Cambridge University Press.

Cook, G., & Walter, T. (2005). Rewriting rites: Language and social relations in traditional and contemporary funerals. *Mortality, 10*(3).

Garcia, C. M., & Reimerink, A. (2022). Cultural context and multi-modal knowledge representation: Seeing the forest for the trees. *Frontiers in Psychology, 13*. https://doi.org/10.3389/fpsyg.2022.824932

Halliday, M. A. K. (1973). *Explorations in the functions of language*. Edward Arnold.

Hatabarat, N. M. P. (2021). Face threatening acts of different ethnic speakers in communicative events of school context. *Pedagogika: Jurnal Ilmu-Ilmu Kependidikan, 1*(1), 17–21.

Isiko, P. A., & Serugo, P. (2021). Death and morality: Perspectives in the moral function of death among the Basoga of Uganda. *EUREKA: Social and Humanities, 5*.

Kasper, G. (1990). Linguistic politeness: Current research issues. *University of Hawai'i Working Papers in ESL, 9*(1), 1–33.

Kibigo, M., Choge, S., & Simiyu, F. (2019). The role of language in facilitating culture: A case study of the Isukha community, Kakamega County in Kenya. *East African Journal of Traditions, Culture and Religion, 1*(2), 16–24.

Kitamura, N. (2000). Adapting Brown and Levinson's "politeness theory" to the analysis of casual conversation. *Griffith Working Papers in Pragmatics and Intercultural Communication, 1*(1), 1–7.

Korir, S. (2021). The effects of burial ceremony in Kenya in the period of COVID-19 pandemic: A case of the Kipsigis community, Bomet County. *International Journal of Novel Research in Humanities and Social Sciences, 8*(4), 43–48.

Lakoff, R. T. (2005). *Language and woman's place*. Harper & Row.

Leech, G. N. (1983). *Principles of pragmatics*. Longman.

Manzu, A., Kamarullah, K., Husda, H., Rasyad, R., & Fauzi, F. (2024). The unity of community in cemetery: An anthropic study of the Islamic burial rituals in Aceh, Indonesia. *Jurnal Ilmiah Islam Futura*.

Mmadike, B. I., & Egenti, M. C. (2016). Speech act analysis of Igbo utterances in funeral rites. *Nsukka Journal of African Studies, 12*, 46–67. https://scispace.com/pdf/speech-act-analysis-of-igbo-utterances-in-funeral-rites-1mryjwnkqw.pdf

Ogola, M. N. (2015). *A study of the neo-traditional death and burial rites among the Luo community in Rarieda: A Christian response* (Unpublished master's thesis). Africa International University.

Ongunyemi, O. (2007). The implications of taboos among African diasporas for the African press in the United Kingdom. *Journal of Black Studies*, 2–22.

Ogunyemi, O. (2007). Retrieved September 21, 2013, from http://online.sagepub.com

Owiredu, C. (2020). Metaphorical conceptions of life and death in the Asante king's burial rites. *Ghana Journal of Religion and Theology, 10*(1).

Qanbar, N. (2011). A sociolinguistic study of the linguistic taboos in the Yemeni society. *MJAL*.

Ryabova, M. (2015). Politeness strategy in everyday communication. *Procedia – Social and Behavioral Sciences*, 206, 90–95.

Shiino, W. (1997). Death and rituals among the Luo in South Nyanza. *African Study Monographs, 18*(3–4), 213–228.

Ushe, M. U. (2017). Rituals and taboos related to death as a repository of traditional African religious ideas: Evidence from the Tiv of Central Nigeria. *IGWEBUIKE: An African Journal of Arts and Humanities, 3*(5).